Chuo Kikuu cha Sokoine
cha Kilimo

# MATUKIO YA SUA


Aprili - Juni, 2024



Ardhi ni Hazina

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 1 | Bodi ya Uhariri. |
| 2 | BITEKO aipongeza SUA kwa mdahalo wa kumuenzi Hayati Sokoine. |
| 4 | Norway yaahidi kuendeleza ushirikiano na SUA. |
| 5 | Balozi wa Ubelgiji Nchini aridhishwa na kazi inayofanywa na Watafiti SUA.<br>Teknolojia ya Malisho SUA ni suluhisho la migogoro ya wakulima na wafugaji. |
| 6 | Maabara ya Mabadiliko ya Mradi wa CLARITY-SUA na utafiti wa kutatua changamoto ya maji Dodoma. |
| 7 | Menejimenti ya SUA yateta na watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda iliyopo mkoani Katavi. |
| 8 | Wahitimu SUA wahimizwa kutumia elimu kwa ubunifu. |
| 9 | Mabalozi wa Nchi za Umoja wa Ulaya watembelea SUA.<br>SUA kuendelea na tafiti kufikisha teknolojia na taarifa kwa kutumia Akili Mnemba. |
| 10 | SUA yatimiza agizo la Rais kushiriki Mkutano wa 11 TAPSEA- Mwanza. |
| 11 | SUA yatoa Mafunzo kwa Vitendo kuendana na Sayansi na Teknolojia. |
| 12 | SUA kukuza ubora wa huduma na uzalishaji bidhaa. |
| 13 | SUA yaahidi kuboresha maslahi ya wafanyakazi wake. |
| 14 | Watumishi SUA wahimizwa kusajili mawazo ya kibunifu. |
| 15 | Wauguzi SUA waaswa kukiishi kiapo chao cha kazi wakati wa utoaji huduma kwa jamii. |
| 16 | SUA, FAO zawanoa wataalam wa Mifugo. |
| 17 | SUA Chuo pekee kinachotoa elimu bora kwa gharama nafuu Afrika. |
| 18 | SUA yapongezwa kuandaa mafunzo kuhusu masuala ya Afya ya Akili. |
| 20 | SUA yapongezwa kuitunza Kampasi ya Solomon Mahlangu. |
| 22 | SUA toeni elimu mliyoipata ya tahadhari na kukabiliana na majanga - Mkaguzi wa Jeshi la Zimamoto. |




## *Bodi ya uhariri*

**Wataalamu wa Mawasiliano na Masoko**

**Bi. Suzana Magobeko**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko

Bw. Asifiwe Mbembela
Afisa Mawasiliano na Masoko

**Mhariri Mkuu**

**Dkt. James Nyangas**
Mhadhiri Mwandamizi

**Mhariri**


**Bw. Absolome Senzige**
Mhadhiri Msaidizi

**Wasanifu**

**Bw. Rajab Kimaro**
**Bi. Jackline Japhet**





*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (Mb) akiongea wakati wa Kongamano la Kumbukizi ya miaka 40 ya Hayati Edward Moringe Sokoine lililofanyika katika Ukumbi wa Multipurpose Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro.*

# BITEKO aipongeza SUA kwa mdahalo wa kumuenzi Hayati Sokoine

Tanzania ina hazina kubwa ya maarifa kutoka kwa viongozi watangulizi akiwemo Hayati Edward Moringe Sokoine.

Hayo yalisemwa April 8, 2024 na Mhe. Dkt. Doto Biteko Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati akihutubia katika Kongamano la kumbukizi ya miaka 40 ya kifo cha Edward Moringe Sokoine lililoandaliwa na Chuo kikuu cha Sokione cha Kilimo ( SUA) Morogoro

Biteko aliipongeza SUA na Wizara ya Elimu kwa kuendelea kuenzi fikra za Hayati Sokoine kwa kufanya mijadala na makongamano yanayoangalia mchango wake katika maendeleo ya Kilimo nchini.

"Nipongeze sana kwa hatua hii ya kuwa na makongamano haya kwa kuwa yanasaidia kujenga uelewa na kutoa historia ya kiongozi wetu mahiri na jinsi alivyochagiza maendeleo ya kilimo ikiwemo kuanzishwa kwa Chuo hiki ambacho kimejikita katika mafunzo ya kilimo" , alisema Biteko

Biteko aliitaka Wizara ya Elimu na SUA kuhakikisha inaweka maandiko ya nasaha na hotuba za Hayati Sokoine kuhusu Kilimo na Maendeleo ikiwemo chambuzi mbalimbali zinazofanywa na Wanataaluma na Viongozi.

"leo hapa tulikua na wanazuoni nguli Prof Shivji , Prof Sibuga na Viongozi wetu Mhe Warioba na Mhe Anna Makinda , tumesikia uchambuzi juu ya Hayati Sokoine fikra, maono, na utendaji wake uliokuwa na weledi mkubwa ni vema hizi kumbukumbu zitunzwe'", aliongeza Biteko

Alikipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwani inawajengea wahitimu ujuzi.

Akizungumza katika Kongamano hilo Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda alisema Vyuo Vikuu nchini vitaendelea kufanya mijadala na chambuzi tunduizi kuhusu nyanja mbalimbali za maendeleo.

"Tunaendelea kuweka msukumo katika mijadala na chambuzi za kitaaluma katika vyuo vikuu, mijadala hii inaelimisha na inatoa pia mawazo chanya kwa ajili ya maendeleo yetu", alisema Prof. Mkenda

Ameongeza kuwa taifa lina mengi ya kujifunza kutoka kwa Hayati Sokoine katika Uongozi na jinsi alivyo chagiza maendeleo ikiwemo kufungua fursa mbalimbali za kilimo biashara.

# *Baadhi ya picha wakati wa Kongamano la Kumbukizi ya miaka 40 ya Hayati Edward Moringe Sokoine 8 Aprili, 2024*



*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (Mb) akiteta jambo na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda wakati wa Mdahalo wa Kumbukizi ya miaka 40 ya Hayati Edward Moringe Sokoine.*

*Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda akitoa neno kwa Wadau waliojitokeza katika Kongamano la Kumbukizi ya miaka 40 ya Hayati Edward Moringe Sokoine.*






*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (Mb) katikati waliokaa, akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wengine wa Serikali na Viongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wakati wa Kongamano la Kumbukizi ya miaka 40 ya Hayati Edward Moringe Sokoine.*

# Norway yaahidi kuendeleza ushirikiano na SUA



***Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda akimkabidhi Balozi wa Norway nchini Tanzania Mheshimiwa Tone Tinnes zawadi mara baada ya kumaliza ziara yake.***

Balozi wa Norway Nchini Tanzania Mheshimiwa Tone Tinnes amesisitiza kuwa taifa la Norway litaendeleza ushirikiano na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, ushirikiano ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 50 mpaka sasa.

Balozi Tone alizungumza hayo katika ziara yake hapa chuoni iliyofanyika tarehe 22 Aprili 2024. Katika ziara hiyo, Mhe. Balozi Tone alifanya mazungumzo na Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda, Menejimenti ya Chuo na watumishi mbalimbali.Wakati wa ziara hiyo Mhe. Tone aliweza kujionea miradi mbalimbali iliyopo SUA inayoendeshwa na kufadhiliwa na



serikali ya Norway ambapo miradi hiyo inaendelea kuleta manufaa kwa jamii wakiwemo wanafunzi wanaosoma katika chuo hicho.

Mhe. Tone alifurahishwa na namna SUA inavyoelimisha watu hususani mabadiliko ya tabianchi. Pia kufundisha watu juu ya kilimo bora na cha kisasa hususani mpango wa mafunzo ya kilimo atamizi na kufanya watu wawekeze kwenye kilimo biashara.

Ameahidi kwa muda wote atakao endelea kuiwakilisha nchi yake hapa Tanzania ataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha na kufanya majadiliano na Makamu Mkuu wa Chuo kuhusu mambo mbalimbali ya maendeleo ya SUA.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda alisema kuwa, ziara hiyo ya Mhe. Balozi Tone ni matokeo ya mkataba wa makubaliano uliosainiwa kati ya SUA pamoja na Chuo Kikuu cha Sayansi za Maisha cha Norway (Norwegian University of Life Sciences) ambapo makubaliano hayo yamelenga katika sekta ya kilimo ili kuwawezesha wakulima kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi lakini pia kuweza kufanya tafiti mbalimbali.

Aidha Prof. Chibunda alisema makubaliano hayo yamelenga pia katika kubadilishana uzoefu vyuo vikuu



vilivyopo nchini pamoja na vyuo vya Norway ikiwemo wataalam mbalimbali wa Vyuo vikuu, walimu, Wanafunzi pamoja na Watafiti ikiwa SUA ni Chuo kimoja wapo katika kufanikisha makubaliano hayo.

Katika ziara hiyo Balozi Tone alitembelea miradi iliyopo chuoni hapo iliyofadhiliwa na Nchi ya Norway, ikiwemo Kituo Cha Taifa Cha kuratibu Hewa Ukaa ya Kaboni.

# Balozi wa Ubelgiji Nchini aridhishwa na kazi inayofanywa na Watafiti SUA



Balozi wa Ubelgiji Nchini Tanzania Mhe. Peter HuygheBaert ameonesha kuridhishwa na kazi inayofanywa na Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo pamoja na Kituo cha Utafiti cha Mradi wa Apopo katika kuhakikisha wanatatua changamoto mbalimbali zinazozikumba nchi mbalimbali duniani ikiwemo kurudisha maeneo ya kuishi kwa usalama kupitia uteguzi wa mabomu.

Alionesha hali hiyo Mei 30, 2024 wakati akiwa kwenye ziara ya siku moja SUA kutembelea miradi yenye ufadhili wa taifa la Ubeligji ambapo amesema kupitia maelezo ambayo amepatiwa na wenyeji wake ameona tija ya miradi hiyo ambayo amekiri kuwa uwepo wake umekuwa na manufaa kwa wananchi hasa mataifa yenye machafuko.

"Kile tulichokiona kinavutia sakutokana na ushirikiano uliopo kwanza kabisa baina ya SUA na Chuo chetu cha Antwerp kwa kushirikiana katika Mradi wakuvutia wa kutumia Panya kwa lengo la kuifanya jamii kuwa salama", alisema Balozi huyo.

Mhadhiri kutoka SUA Prof. Abdul Katakweba akimuwakilisha Prof. Allen Malisa Mkurugenzi wa Taasisi ya Kudhibiti Viumbe Hai Waharibifu alisema APOPO inafanya kazi chini ya SUA lakini pia kuna ushirikiano baina ya SUA, APOPO pamoja na Chuo Kikuu cha Antwerp kilichopo nchini Ubelgiji.

Alisema APOPO ni Taasisi isiyo ya Kiserikali kutoka nchini Ubelgiji na Ubalozi wa Ubelgiji ndio unaofadhili sehemu kubwa ya tafiti zinazofanywa na shirika hilo pamoja na SUA. Hivyo, ujio wa balozi ni kujiridhisha kwa kuangalia kama misaada inayotolewa na nchi yao inafanya kazi vizuri na kitu kizuri ni kuwa kazi imeonekana.

# Teknolojia ya Malisho SUA ni suluhisho la migogoro ya wakulima na wafugaji




***Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Tanga Ustadhi Rajabu Abdallah akipata maelezo kwa Wataalamu alipotembelea Banda la SUA katika Maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu.***

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Tanga Ustadhi Rajabu Abdallah, amesema teknolojia ya malisho iliyofanyiwa utafiti Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ni suluhisho la mapigano ya wakulima na wafugaji.

Ustadhi Rajabu Abdallah alisema hayo alipotembelea Banda la SUA katika Maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu iliyoanza tarehe Mei 25, 2024 jijini Tanga.

Alisema katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo mkoa wa Tanga kumekuwa na ugomvi wa mara kwa mara wa mapigano kati ya wakulima na wafugaji kutokana na mifugo kula mazao ya wakulima wakati wa malisho.

Ustadhi Abdallah alisema teknolojia ya malisho ambayo mfugaji anaweza kuwa na eneo lake na kupanda malisho ambayo hustawi vema inaweza kuondoa migogoro baina ya wakulima na wafugaji.



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam), Prof. Maulid Mwatawala akifungua Warsha ya Maabara ya Mabadiliko chini ya Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Ustahimilivu katika Nyanda Kavu za Kitropiki (CLARITY).*

# Maabara ya Mabadiliko ya Mradi wa CLARITY-SUA na utafiti wa kutatua changamoto ya maji Dodoma

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kimeendelea kufanya tafiti ili kupata majawabu ya changamoto mbalimbali za upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma kwa kutumia Maabara ya Mabadiliko (Dodoma Transformation lab).

Kauli hiyo ilitolewa Juni 20, 2024 jijini Dodoma na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam, Prof. Maulid Mwatawala wakati akifungua Warsha ya Maabara ya Mabadiliko chini ya Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Ustahimilivu katika Nyanda Kavu za Kitropiki (CLARITY).

Prof. Mwatawala alisema pamoja na SUA kutoa Astashahada na Shahada mbalimbali za Uzamili na Uzamivu, pia kinafanya tafiti zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali nchini ikiwemo changamoto ya upatikanaji wa maji. Madhara ya changamoto yamekuwa dhahiri katika maeneo mengi ya nchi na kwamba hali inaweza kuwa mbaya zaidi kwenye maeneo ya nyanda kavu na kame za kitropiki kama mkoa wa Dodoma.

"Mradi huu unatumia njia ya Maabara za Mabadiliko (Transformation labs) ambayo inatoa fursa muhimu kwetu sote kufanya kazi kwa pamoja na kuchukua jukumu la kutafuta suluhisho la upatikanaji wa maji ya uhakika, endelevu na usawa katika jiji la Dodoma.

"Tafiti na uzoefu kutoka nchi zingine kwenye maeneo yenye hali sawa na ya Dodoma unaonesha kuwa maji chini ya ardhi mara nyingi husaidia kupunguza madhara yatokanayo na athari za ukame na mabadiliko mengine ya tabianchi , hivyo ni matumaini yetu kuwa Mradi huu wa CLARITY utakuwa suluhisho la upatikanaji wa maji katika jiji hili", alisema Prof. Mwatawala.

Akizungumzia kuhusu mradi huo Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu, na Mkuu wa Mradi huo Prof. Japhet Kashaigili alisema malengo mahususi ya Mradi wa CLARITY ni kubaini changamoto na suluhisho bunifu kupitia utafiti wa kitaalamu katika fani mbalimbali ambapo malengo ya utafiti huo yanatarajiwa kufanikiwa kupitia Maabara za mabadiliko.

"Tunaposema Maabara ya mabadiliko tuna maana kuwa hii ni nafasi jumuishi, salama, ambayo wadau, watafiti na wataalamu wanakutana pamoja kufanya majaribio kupima na kubadilishana mawazo na kushirikiana katika kuzalisha maarifa na kutathmini suluhu zake", alisema Prof. Kashaigili.

Akitoa neno katika warsha hiyo Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kutoka Wizara ya Maji Dkt. George Lugomela alisema ili kukabiliana na hali hii kuna umuhimu mkubwa wa kufanya tafiti ili kubaini namna bora ya kusimamia vyanzo hivi vya maji ili visiendelee kuchafuliwa ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa wizara pamoja na bodi za mabonde ya maji.



# Menejimenti ya SUA yateta na watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda mkoani Katavi



*Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ikiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda (katikati, waliokaa) katika picha ya pamoja na Watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda.*

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda amefanya ziara katika Kampasi ya Mizengo Pinda ili kujionea maeneo ambayo yatakwenda kujengwa majengo matatu kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), ambapo litajengwa Jengo la taaluma, bwalo na daharia.

Prof. Chibunda aliwataka watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda Kushirikiana katika kazi na kuendeleza utamaduni wa SUA kuwa mfano wa kuigwa kwa jamii inayotuzunguka.

Kwa upande wake Naibu Mratibu wa Mradi Dkt. Winfred Mbungu alisema Mradi huu unadhamini mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ambapo amewataka watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda kutumia fursa hiyo kujiendeleza kielimu, huku akibainisha baadhi ya watumishi waliopata udhamini wa kielimu kupitia mradi huo.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Utawala na Fedha) Prof. Amandus Muhairwa aliwataka watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda kutumia vyema ofisi za viongozi pindi wanapokuwa na changamoto au wanapohitaji kupata ufafanuzi wa taarifa yeyote inayomuhusu mfanyakazi husika na kuacha tabia ya kuziogopa ofisi hizo.

Kwa Upande mwingine Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam) Prof. Maulid Mwatawala aliwakumbusha Wanataaluma kuzingatia misingi ya ufundishaji kwa kufuata utamaduni, utaratibu na miongozo ya Chuo katika kufundisha ili kuzalisha wataalamu wenye tija katika taifa letu.

Pia, Prof. Mwatawala alisema kuwa Chuo kipo katika zoezi la kuboresha mitaala ya Chuo, ambapo alisema Kampasi ya Mizengo Pinda wamelenga kuongeza baadhi ya kozi zitakazoongeza idadi ya wanafunzi katika Kampasi hiyo na kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika jamii inayozunguka Chuo na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Baada ya mkutano huo na watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda, Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo walipata fursa ya kutembelea maeno yatakapojengwa majengo matatu.



*Naibu Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), Dkt. Winfried Mbungu akielezea maendeleo ya mradi huo*

# Wahitimu SUA wahimizwa kutumia elimu kuwa wabunifu



*Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman akihutubia wakati wa Mahafali ya 43 ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo iliyofanyika Kampasi ya Edward Moringe 23 Mei, 2024.*

Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo (SUA) wameaswa kutumia elimu na mafunzo waliyopata chuoni hapo kwa ubunifu katika kufanya ubunifu wa maendeleo endelevu kwa ustawi wa taifa la Tanzania.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman wakati akitoa hotuba kwenye mahafali ya 43 ya katikati ya mwaka ya Chuo yaliyofanyika kwenye Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro ambapo zaidi ya wanafunzi 700 wamehitimisha safari ya masomo yao.

Alisema kwa niaba ya Baraza la Chuo wanakusudia kuona ubunifu kwa wahitimu kwenye shughuli ambazo watakuwa wanafanya ili kuleta tija katika maisha yao kiuchumi, kitaaluma na manufaa kwa taifa kwa ujumla.

"Mnapoingia kwenye ulimwengu wa ajira iwe ya kuajiriwa au ya kujiajiri kumbukeni kuwa nyinyi ni mabalozi wetu katika kutunza maadili ,ubunifu, na uchapakazi, maarifa na ujuzi mlioupata hapa ziwe dhana za kuleta mabadiliko chanya kushughulika na matatizo ya nchi na za kimataifa na kuboresha maisha ya watanzania na jamii kwa ujumla," alisema Mhe. Chande

Aidha, aliwataka wahitimu kuyaishi maneno ya Hayati Nelson Mandela, Rais wa Kwanza wa Afrika ya Kusini ambayo yanasema elimu ndiyo silaha yenye nguvu zaidi ambayo inaweza kutumia kubadilisha ulimwengu na anaamini kuwa wahitimu hao wana uwezo wa kuubadilisha ulimwengu.

Goodluck Saltiel Maoy mhitimu wa Shahada ya Uhifadhi wa Wanyamapori SUA aliipongeza Menejimenti ya Chuo kwa kuandaa sherehe za mahafali ya katikati ya mwaka huku akiwataka wahitimu wenzake kuyaishi kwa vitendo yale yote ambayo wamejifunza katika kipindi chote cha maso-














# Mabalozi wa Nchi za Umoja wa Ulaya watembelea SUA.

Waheshimiwa Mabalozi wa Nchi za Umoja wa Ulaya walitembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kujionea miradi mbalimbali inayoendelea chuoni hapo kwa ufadhili wa Nchi Wanachama wa Jumuiya hiyo.

Mabalozi hao wakiongozwa na Balozi wa Jumuiya ya Ulaya na Jumuiya ya Afrika Mashariki Mhe. Christine Grau, walipokelewa chuoni hapo na Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda na kupata fursa ya kufanya mazungumzo na Menejimenti ya Chuo.

Katika ziara hiyo Waheshimiwa Mabalozi walitembelea Kituo Cha Taifa Cha Kuratibu Hewa Ukaa ya Kaboni.
na Kituo cha Kufundishia Panya (APOPO).

Naye Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, upande wa Mipango , Fedha na Utawala, Profesa Amandus Muhairwa, amesema Mabalozi hao wameridhika na kinachofanyika SUA na hivyo kuweza kuendelea na mahusiano wakiwa ni wafadhili wa miradi mbalimbali.

“Hii imekuwa ni nafasi ya kuonesha tuliyoyafanya na kuendeleza mahusiano na wafadhili kwa faida ya nchi na faida kwa vijana ambao ni wanufaika katika kutengeneza ajira ambalo ni lengo la miradi mingi inayofanyika chuoni” alizungumza Profesa Muhairwa.

Kiongozi wa Mabalozi, Mhe. Christine Grau amesema, wamefurahishwa na maendeleo ya miradi inayofanywa na SUA. Pia amewataka vijana wa Kitanzania ambao wamepata fursa ya kufikia Elimu ya Juu kutumia muda wao vizuri ili waweze kufaulu masomo na kutatua changamoto za jamii wanazotoka ikiwepo suala la athari ya mabadiliko ya tabianchi.

## SUA kuendelea na tafiti kufikisha teknolojia na taarifa kwa kutumia Akili Mnemba

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimesema kinaendelea kufanya tafiti mbalimbali ikiwemo matumizi ya Akili Mnemba ili kurahisisha mawasiliano na upatikanaji teknolojia za kilimo na taarifa sahihi zinazoweza kuwasaidia wakulima katika kutatua changamoto zao.

Hayo yalisemwa Mei 25, 2024 na Mkuu wa Kitengo cha Ugani kutoka Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza ICE, SUA Dkt. Emmanuel Malisa katika maonesho ya Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyoanza jijini Tanga.

Dkt. Malisa alisema matumizi ya Akili Mnemba na mawasiliano rahisi, yakiwa ni pamoja na kutumia simu za mkononi za aina zote baina ya mkulima na wataalamu kwa kutumia teknolojia hiyo ya mawasiliano itatatua changamoto nyingi.

"Sasa tunataka kufikia hatua ya kutumia Akili Mnemba kuhakikisha kuwa mkulima yeyote ambaye ana simu yake mahali popote anaweza kupata teknolojia au taarifa iliyotokea SUA kwa wakati, tayari tumeanza tafiti kidogo kidogo na tunaamini watafiti wetu watakamilisha hilo” alisema Dkt. Malisa.






# SUA yatimiza agizo la Rais kushiriki Mkutano wa 11 TAPSEA- Mwanza

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeendelea kuunga mkono Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alilolitoa katika Mkutano wa 10 mjini Zanzibar la waajiri kuwapa nafasi ya kushiriki mikutano ya kitaifa ya Makatibu Mahsusi Tanzania (TAPSEA), ambapo mwaka 2024 SUA ilituma washiriki katika Mkutano wa 11 uliofanyika jijini Mwanza na Mgeni Rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko.

Katika kutimiza agizo hilo la Rais Samia Menejimenti ya SUA ilitoa zaidi ya shilingi Milioni 40 kwa Makatibu Mahsusi 25 kushiriki mkutano huo na taratibu nyingine zilizowawezesha kushiriki vikao hivyo vya kitaaluma na Mkutano Mkuu wa 11 uliofanyika siku ya Jumamosi tarehe 25/05/2024.

Aidha kwa siku zote kuanzia tarehe 20-24 shughuli hizo zilifanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza zikihusisha mada mbalimbali katika kuwajenga kitaaluma, kuwakumbusha wajibu wao katika kazi pamoja na kuzingatia maadili na uadilifu wawapo kazini ikiwemo usimamizi wa mikataba ya utendaji, ushughulikiaji wa mrejesho, muundo wa maendeleo ya utumishi wa kada ya waendesha ofisi.

Mkutano huo wa 11 ulibeba Kauli Mbiu isemayo *"Mafanikio Huanza na Uamuzi Bora wa Utendaji, Tutumie Muda Vizuri kwa Kufanyakazi na Kuleta Tija"*.





# SUA yatoa Mafunzo kwa Vitendo kuendana na Sayansi na Teknolojia

*Kutokana na ukuaji wa Sayansi na Teknolojia katika kilimo duniani Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kinaendelea kuwafundisha wanafunzi wake kwa vitendo kupitia mashamba na bustani za Kilimo cha Matunda na Mboga namna bora ya kuweza kutumia fursa hiyo ili kuwa bora katika ajira au kujiajiri wenyewe.*

*Akizungumza na SUA MEDIA kuona namna ambavyo matumizi ya Teknolojia za Kilimo zinawezaje kumsadia mwanafunzi awapo katika mafunzo kwa vitendo chuoni hapo, Afisa Kilimo Mwandamizi toka Idara ya Mimea Vipando na Bustani Bw. Godwin Rwezaula alisema kuwa Chuo kinaendelea kuboresha na kuongeza vitendea kazi kulingana na mahitaji ya ufundishaji kutokana na hali ya sasa wanafunzi wanatakiwa kuzifahamu teknolojia mpya na matumizi yake hata kabla hawajahitimu.*

*Afisa Kilimo huyo aliongeza kuwa suala la kuamua wanafunzi kufanya Mafunzo kwa Vitendo chuoni hapo limekuwa na faida kwa wanafunzi hivyo kupelekea idadi ya wanafunzi kuongezeka ambapo zaidi ya wanafunzi elfu mbili kutumia mashamba na bustani za chuo kwa kufanyia Tafiti na Kilimo tofauti na miaka ya nyuma.*

*Naye mwanafunzi wa mwaka wa tatu wa Shahada ya Kilimo chuoni hapo Bw. Hassan Mohamed alielezea faida wanayopata kupitia chuo hicho na kusema kuwa mafunzo hayo yanayozingatia ulimwengu wa Teknolojia katika upande wa kilimo kwao ni faida ambayo inawafanya wakimaliza masomo yao kuweza kuelimisha jamii kuhusiana na umuhimu wa kutumia teknolojia katika kilimo kwa kuwa maeneo wanayotoka elimu hiyo haipo na wakulima wengi wanalima kimazoea.*

*Alizitaja faida wanazozipata kama vile mafunzo ya kutumia mbegu sahihi, kilimo na uvunaji wenye tija, kurahisisha umwagiliaji maji au dawa kwa kutumia ndege (drone), kuongeza uzalishaji wa mazao, utambuzi wa vifaa vya kurahisishia kazi, pamoja na kutunza mazingira kwa kuacha kuchoma moto eneo kwa matumizi ya kilimo.*

*Aidha Bw. Mohamed alisema kuwa elimu wanayopata itasadia kuwakumbusha wazazi watumie fursa hiyo ya ukuaji wa teknolojia kwa kuwafanya watoto wao wajiunge na SUA kusomea kilimo kwani sekta ya kilimo kwa sasa inahitaji watu wenye utaalamu hata kama hawakuweza kuajiriwa wawe wanauwezo kujiajiri wenyewe na kuepukana na utegemezi kwa kusubiri ajira.*

*Aidha aliwaasa wanafunzi wenzake kutambua kuwa wao ni mabalozi kutoka SUA hivyo kufanya kwao kazi vizuri katika jamii ndio inaleta hamasa kwa wengine kupenda kilimo wasione shida kujitolea kufanya kazi hizo kwani zinawajenga kuwa bora.*









Rasi wa Ndaki ya Uchumi na Stadi za Biashara kutoka SUA, Dkt. Damas Philip.

# SUA kukuza ubora wa huduma na uzalishaji bidhaa

Wafanyakazi katika vitengo vya uzalishaji Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), wametakiwa kuzingatia mafunzo waliyopata ili kukuza ubora wa huduma na bidhaa zinazotolewa SUA.

Hayo yalisemwa na Rasi wa Ndaki ya Uchumi na Stadi za Biashara kutoka SUA Dkt. Damas Philip alipokuwa akizungumza na washiriki wa mafunzo hayo kutoka vitengo zaidi ya 45 vya uzalishaji walioshiriki mafunzo ya siku mbili katika Kampasi ya Edward Moringe mkoani Morogoro.

Alisema SUA ni miongoni mwa Taasisi za Serikali zenye rasilimali nyingi ambazo zinatakiwa kutumiwa kwa usahihi ili kuleta tija chuoni na taifa kwa ujumla kwa kuongeza uzalishaji katika vitengo vilivyopo ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji.

"Nimefurahi kusikia kuwa wawezeshaji ambao wametumika katika mafunzo haya wametoka ndani ya chuo ambao wanakifahamu chuo vizuri na fursa zilizopo na hii imeonyesha namna nzuri ya kutumia rasilimali tulizonazo kwa kuleta maendeleeo kwa taasisi na nina amini mafunzo haya ya siku mbili hayajapotea bure na kila kitu kitatiliwa maanani ", alisema Dkt. Philip.

Naye, Suma Mwakanenela kutoka Ndaki ya Uchumi na Stadi za Biashara ambae alikuwa muwezeshaji wa mafunzo hayo, alisema kuwa mafunzo hayo yatasaida kukuza uzalishaji katika vitengo mbalimbali ndani ya SUA, iwapo yatafanyiwa kazi kwa kuongeza ubora kwa kutumia ubunifu na fursa ipasavyo ili kuongeza uzalishaji.

Kwa upande wake mmoja wa washiriki katika mafunzo hayo Bakari Mohamed Abdallah kutoka Shule Kuu ya Uhandisi na Teknolojia (SoET) aliwashukuru, waandaaji wa mafunzo hayo kwa kuwaongezea uelewa wa namna nzuri ya kutumia fursa na amekiri kujua vitu vingi ambavyo awali hakuwa akivijua mfano matumuizi ya busara katika utoaji huduma kwa wateja.

Naye Grace Kajuna Afisa Utumishi kutoka Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza, ICE SUA alisema mafunzo hayo yamemuongezea uelewa hasa namna mzuri ya kutumia fursa zilizopo kwenye kuongeza pato la Chuo na anatatarajia kuboresha huduma anazozifanya katika kitengo chake na ameahidi kuyatekeleza yote aliyojifunza katika uzalishaji.





*Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda akimkabidhi cheti mmoja wa Watumishi waliochaguliwa kuwa Wafanyakazi bora.*

# SUA yaahidi kuboresha maslahi ya watumishi wake

Menejiment ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imeahidi kuboresha maslahi ya wafanyakazi kulingana na bajeti kwa kuanza na wafanyakazi waendesha ofisi, wahudumu na usalama katika chuo hicho kwa kuwaongezea kipato (Posho) kwa lengo la kuwafanya waongeze bidii, nidhamu na uaminifu katika kazi zao.

Akizungumza na wafanyakazi katika kilele cha Siku ya Wafanyakazi Mei Mosi, Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda alisema kada hizo zimekuwa zikifanya kazi lakini mapato yao ni madogo hivyo kwa kuhakikisha nao wanaweza kupata ongezeko, Chuo kimeamua kuanza nao wakati kikiendelea kujipanga hadi kufikia kila mfanyakazi katika kada nyingine chuoni hapo.

Akijibu ombi la wafanyakazi kupatiwa usafiri lilisomwa katika risala yao Prof. Chibunda alisema kuwa tayari chuo kimeongeza mabasi kwa ajili ya wanafunzi hadi kufikia saba, lakini pia wameona kuna uhitaji wa kuongeza mabasi zaidi kwa ajili ya wafanyakazi kulingana na gharama za maisha na nauli kupanda ili kila mfanyakazi apate huduma ya usafiri.

Aidha alisema kuwa yote hayo yanafanyiwa kazi na Menejimenti lakini wanataka kuona wafanyakazi wanafanya kazi kwa bidii, uaminifu, uadilifu na uzalendo katika chuo hicho, na kusema kuwa wafanyakazi watambue wanawajibu kufanya hivyo na sio suala la kusukumwa katika kuwahi kufika kazini, kuhakikisha wanafanya kazi kikamilifu, pamoja na kufahamu utaratibu wa kupata likizo na malipo ya likizo zao ili kuepuka malalamiko mbalimbali.

Prof. Chibunda pia aliwapongeza wafanyakazi bora 74 wakiwemo wanataaluma na waendeshaji katika chuo hicho kwa kuwapatia zawadi za fedha na vyeti, ambapo wawili kati yao ambao ni wafanyakazi bora wa Chuo wamepata zawadi katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi ki mkoa yaliyofanyika wilayani Ifakara mkoani Morogoro na kusisitiza kuwa, kila mfanyakazi katika nafasi yake kuwajibika ipasavyo ili kuleta maendeleo ya chuo na taifa kwa ujumla.



# Watumishi SUA wahimizwa kusajili mawazo ya kibunifu



Watumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wamehimizwa kusajili mawazo ya kibunifu ambayo wanayamiliki ili yaweze kulindwa kisheria na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Wito huo ulitolewa na Msajili Msaidizi wa Kurugenzi ya Miliki Bunifu kutoka BRELA Bi. Neema Mtala wakati wa mafunzo hayo SUA Aprili 19, 2024 ambapo amesema kutokana na majukumu ya watumishi wakiwemo Wahadhiri katika Vyuo mbalimbali nchini ya kufanya tafiti ambazo huzalisha mawazo ya kibunifu wanatakiwa wasajili mawazo hayo ili yaweze kulindwa kisheria.

Bi. Neema alisema mawazo ya kibunifu yanapolindwa kupitia sheria na taratibu za BRELA inakuwa rahisi kuwa kwenye umiliki wa mbunifu huyo tofauti na mawazo hayo kuuanza kutoa huduma bila kusajiliwa.

"Kabla ya kupeleka bunifu yako sokoni ni muhimu kuirasimisha kwetu (BRELA), maana tuna mamlaka ya kuitunza na kuilinda huduma, hataza na biashara za waanzilishi husika kupitia sheria mbalimbali zilizoundwa", alisema Bi. Neema.

Aliongeza kutokana na elimu ambayo wameitoa wanaamini watumishi hao sasa wataanza kurasimisha mawazo ya kibunifu, usajili wa alama za biashara, huduma pamoja na hataza kabla ya kupelekwa sokoni na kwamba kwa kufanya hivyo itaongeza usalama wa juhudi ambazo zinawekwa wakati wa uvumbuzi.

Kwa upande wake Dkt. Doreen Ndossi, Mratibu wa Kitengo cha Uhawilishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu kutoka SUA alisema elimu ambayo wameipata itakuwa chachu kwa watumishi na Taasisi kwa ujumla kusajili BRELA na kubiasharisha mawazo ya kibunifu ili yaweze kulindwa kisheria.

Dr. Ndossi alisema hali ya urasimishaji wa bunifu za wataalamu wa SUA bado ziko chini lakini Chuo kina hataza mbalimbali ambazo zimefanywa hivyo kupitia elimu ambayo imetolewa itaweza kusaidia zaidi.

Mmoja wa washiriki Bw. Julius Luvanga alisema mafunzo hayo ni muhimu kwao kama Wanataaluma kwani yanawaongezea uelewa wa namna ya kulinda mawazo ya kivumbuzi na yamewapa uzoefu wa namna ambavyo watalinda huduma na usajili wa alama za biashara zao.






*Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Huduma za Afya SUA, Dkt. Omary Kasuwi (wa nne kushoto) katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa Kurugenzi hiyo.*

# Wauguzi SUA waaswa kukiishi kiapo chao cha kazi wakati wa utoaji huduma kwa jamii

Wauguzi katika Hospitali za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wametakiwa kuzingatia viapo vyao kwa kutoa huduma bora kulingana na maadili ya kazi kwakuwa umuhimu wa kazi hiyo ndio unaowatofautisha na kazi zingine ambazo hazitoi viapo kwa taaluma zao.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Huduma za Afya SUA Dkt. Omary Kasuwi wakati akihitimisha Wiki ya Wauguzi ambapo wauguzi kutoka SUA wameungana na wauguzi kote duniani, wakiadhimisha wiki hiyo kwa kufanya vipimo na ushauri, usafi katika jamii na kutoa zawadi mbalimbali kwa wagonjwa hospitalini hapo.

"Ndugu zangu nyinyi lazima mtambue kuwa sio kila taaluma wanapewa viapo vya kazi, kiapo ni kitu kikubwa sana kwa mtu au taaluma ndio maana unaweza kuona ni taaluma chache sana zinazotoa viapo, Kiapo kina maana kubwa sana kiroho na kimaadili katika utoaji wa huduma hivyo pamoja na changamoto mbalimbali mnazokabiliana nazo lakini niwakumbushe kuviishi viapo vyenu " alisema Dkt. Kasuwi.

Mkurugenzii huyo alisema kuna jitihada kubwa zinafanywa kupitia hospitali na Menejimenti ya SUA katika kupunguza baadhi ya changamoto walizoainisha hivyo amewataka kuendelea kufanya kazi kwa moyo kuhudumia jamii na pindi fedha zitakapopatikana changamoto hizo ikiwemo uchache wa watumishi na mahitaji mengine yatatatuliwa ili kuzidi kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Kwa upande wake Matroni wa Hospitali za SUA Bi. Akaanashe Makere alipongeza Menajimenti ya SUA kupitia kwa Dkt. Kasuwi kwa namana anavyopigania Kurugenzi ya Afya chuoni hapo na fani ya uuguzi kwa pamoja, kwa kuweka kipaumbele zaidi kuona huduma bora zinatolewa kwa wanaohitaji taaluma yao, hasa katika kupigania upatikanaji wa madawa na vifaa tiba na utoaji huduma unakuwa rafiki kwa wafanyakazi wote ambapo jumla ya watu 62 walipimwa katika kipindi cha wiki moja.

"Umekuwa ukijitolea muda wako mwingi sana kutupatia elimu sehemu za kazi ili kuboresha utendaji wetu hivyo tunakuahidi kuwa tutazidi kufanyia kazi yale yote unayotuelekeza na tutakuwa bora zaidi. Lakini niwatake pia wauguzi wenzangu kujiendeleza katika nyanja mbalimbali pale fursa inapopatikana na tutumie mitandao kujiendeleza na masomo tunayopata mara kwa mara wakati wa vikao vya kila siku asubuhi kwaajili ya kupata alama za kuhuisha leseni zetu" Alieleza Matroni Makere.

# SUA, FAO zawanoa wataalam wa mifugo




*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Charles Mhina akifungua mafunzo kwa wataalamu wa Tiba za wanyama Tanzania Bara na visiwani.*

Wizara ya Kilimo na Uvuvi kwa kushirikina na Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) wameendesha mafunzo kwa wataalamu wa Tiba za wanyama Tanzania Bara na visiwani katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) yenye malengo ya kukuza uelewa katika sayansi ya wanyama Tanzania.

Mafunzo hayo yalifunguliwa na Dkt Charles Mhina ambae ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Washiriki zaidi ya 30 walipata mafunzo hayo yaliyofanyika ndani ya Kampasi ya Edward Moringe mkoani Morogoro kwa siku thelathini na wiki moja ya kwenda uwanjani kujifunza kwa vitendo.

Dkt Mhina alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatambua umuhimu mkubwa wa kilimo na mifugo nchini katika kukuza ubora wa afya za jamii kwa kuboresha mazingira mazuri kwa wanyama huku lengo kuu likiwa ni kupata tija kupitia mifugo hiyo kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla na serikali itahakikisha kuwa mafunzo haya yatakuwa endelevu ili kuendelea kukuza uelewa kwa wataalamu wote nchini.

Pia alitoa shukrani kwa SUA na FAO kwa kutoa ushirikiano wao thabiti na serikali kwa kuendelea kutoa mafunzo endelevu kwa wataalamu wa afya ya wanyama na binadamu nchini kwa kushirikiana na serikali kwa lengo la kuisadia jamii kuondokana na changamoto katika sekta ya uvuvi na mifungo ikiwemo magonjwa ya mlipuko kwa kuyatafutia ufumbuzi wa haraka.

Naye, Prof. Ezron Karimuribo Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya kutoka SUA aliupongeza uongozi wa chuo kwa kuendelea kuwa wadau wakubwa katika utoaji wa mafunzo kwa wataalamu wa mifugo na kuongeza kuwa katika mafunzo haya SUA imeusika katika kuandaa mtaala na mafunzo hayo. aliwataka washiriki wote kuyafanyia kazi yale yote waliyojifunza katika kipindi chote cha mafunzo ili kuleta tija kwa taifa.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo ni mazuri kwa sababu yatasaidia kutambua changamoto zinazowakabili wanyama kwa haraka na kuanza kuchukua tahadhari.

Kwa upande wake, Zehra Zam kutoka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kutoka Zanzibar alisema mafunzo hayo yatasadia kukuza ubora wa huduma wanazozitoa kwa jamii na ametoa rai kwa wafugaji wote nchini kuwa makini katika kuzingatia hali ya usafi ndani ya kipindi cha mvua kwa mifugo yao kwa kuhakikisha uwepo wa chakula bora, matibabu na mazingira mazuri wanayoishi wanyama hao ili mifugo iweze kuwa na afya bora itakayokidhi ubora wa kimataifa.



*Washiriki wa mafunzo wakiwa katika picha pamoja na mgeni rasmi katika Kampasi ya Edward Moringe mkoani Morogoro.*

# SUA Chuo pekee kinachotoa elimu bora kwa gharama nafuu Afrika



Katika kuhakikisha ushirikiano na mawasiliano mazuri kati ya wanafunzi wa ndani na nje ya nchi, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeamua kupunguza gharama za ada kwa wanafunzi wa kimataifa na kufanya chuo hicho kuwa pekee kinachotoa elimu yenye ubora kwa gharama nafuu Afrika kwa lengo la kuendelea kuvutia watu wote duniani kujiunga na chuo hicho.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Prof. Maulid Mwatawala alisema wanafunzi wote katika Jumuiya ya Africa mashariki wamepata punguzo la Ada kwani wameamua kutoa elimu bila kujali utaifa na kuendelea kufanya chuo hicho kuwa na hadhi ya kimataifa kwa kimeweka miundombinu rafiki kwa wote wanaopata nafasi ya kusoma hapo.

Prof. Mwatawala alisema Chuo kinaendelea kuhimarisha ubora wa elimu kwa kupitia mitaala na kufanya elimu inayotolewa hapo kuwa kwa vitendo zaidi pamoja na kuhakikisha mahitaji muhimu ya wanafunzi wote yanapatikana kikamilifu ili waweze kuishi vizuri wawapo chuoni kwani nchi ya Tanzania ina makabila zaidi ya 120 hivyo amewataka wanafunzi hao kutumia fursa hiyo kwa kujifunza Kiswahili wasichukulie hiyo kama ni changamoto kwao bali fursa na hiyo ndio maana halisi ya kimaifa.

Kupitia siku hiyo mataifa mbalimbali yaliweza kuonesha tamaduni zao kwa mavazi, kuelezea historia ya mataifa yao, chakula, pamoja na kufurahia nyimbo na kucheza kitamaduni ambapo wanafunzi 105 wakiwemo kutoka nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Lesotho, Comoro, Zimbabwe, Mauritius, Afrika ya Kusini na Botswana.

Na wengine ni kutoka nchi za Liberia, Ethiopia, Eswatini, Namibia, Congo, Benin, Nigeria na Msumbiji wameweza kuonesha namna wanavyoweza kucheza kitamaduni. Pia washiriki wakiongozwa na Mgeni rasmi walionja vyakula vilivyopikwa kutoka mataifa mbalimbali ulimwenguni.







*Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Morogoro anayehusika na Rasilimali Watu Bw. Herman Tesha (katikati waliokaa) katika picha ya pamoja na viongozi wengine wa Serikali na viongozi wa Chuo Kikuu cha Sokine cha Kilimo akiwemo Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala) Prof. Amandus Muhairwa (wa pili kushoto waliokaa).*

# SUA yapongezwa kuandaa mafunzo kuhusu masuala ya Afya ya Akili

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimepongezwa kwa kuandaa mafunzo maalumu kuhusu masuala ya afya ya akili kwa watumishi wa Chuo.

Pongezi hizo zilitolewa na Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Morogoro anayehusika na Rasilimali Watu Bw. Herman Tesha wakati akifungua mafunzo hayo ya siku mbili yaliyofanyika Ukumbi wa Multipurpose Juni 24, 2024 na Juni 25 kwa Kampasi ya Solomon Mahlangu.

Bw. Herman alisema mafunzo ya afya ya akili kwa watumishi ni muhimu kwani yana nafasi kubwa katika kuongeza ari na ufanisi katika utumishi wa wafanyakazi kwenye maeneo yao.

"Kunapokuwa na mafunzo kama haya hususan kwenye eneo la afya ya akili unategemea ufanisi kuongezeka, msongo wa mawazo kwa watumishi utaondoka na eneo la kazi litasalia kuwa salama", alisema Bw. Herman

Mwezeshaji wa mafunzo hayo Daktari. Bingwa Mbobevu kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Garvin Kweka, alisema mafunzo ya afya ya akili ni lazima kwa watumishi na jamii kwa ujumla ili kujenga jamii iliyo bora na isiyo na matukio ya ajabu, akitolea mfano wa baadhi ya matukio ya kikatili yaliyoweza kutokea nchini na kufanywa na watumishi wa serikali.

Pia, aliwataka watumishi kuwa na tabia ya kuweka wazi mambo yanapokuwa hayaendi sawa ili waweze kusaidiwa kuliko kubaki nayo, suala linaloongeza matukio ya kujiua.

Akizungumza kwa niaba ya Chuo, Mkuu wa Menejimenti Rasilimali Watu na Utawala Peter Mwakiluma alisema walianza na mafunzo kwa menejimenti baada ya kuona umuhimu wake wakaona ni vyema watumishi wote kupatiwa mafunzo ya afya ya akili.



## *Wanafunzi wa SUA wakiwa katika maeneo mbalimbali ya Hifadhi za Taifa kama sehemu ya Mafunzo kwa Vitendo*











# SUA yapongezwa kwa kuitunza Kampasi ya Solomon Mahlangu

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimepongezwa kwa kuifanya Kampasi ya Solomon Mahlangu kuwa kituo cha mafunzo ambacho kinawasaidia vijana wa Kitanzania kufikia malengo yao kitaaluma huku miundombinu ikiendelea kuhifadhiwa kwa ajili ya historia na alama ya uhusiano wa kindugu, kirafiki na ushirikiano kati ya Tanzania na Afrika ya Kusini.

Alibainisha hayo Bw. Spencer Hodgson mmoja wa wasanifu wa majengo na miundombinu wakati wa harakati za ukombozi wa Afrika ya Kusini alipotembelea katika Kampasi ya Solomon Mahlangu mjini Morogoro Juni 10, 2024 ambapo amesema sehemu hiyo ni ya muhimu kwa maisha yao kwa kuwa waliishi katika eneo hilo.

Alisema amefurahi kuona eneo hilo lililokuwa pori sasa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, akisema wakati wanaondoka maeneo mengi yalikuwa wazi kwa lengo la kuwasaidia kuona adui na kukimbia ambapo sasa eneo hilo limeboreshwa na kuendelezwa katika historia.

"Nimefurahi kuja Tanzania hususani katika eneo ambalo lilikuwa sehemu ya maisha yangu, nimetembea na kuona jinsi eneo lilivyoboreshwa zaidi kwa kujengea majengo mapya, kupanda miti na kuitunza vizuri sehemu hiyo ya kihistoria inapendeza sana. Hapa ndipo mahali tulipoanzia na baadaye kwenda Dakawa hivyo nasikia fahari kuwa mahali hapa", alisema Hodgson.

Naye mwenyeji wake Dkt. Geoffrey Karugila kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda alisema kuwa ujio wa wageni mbalimbali kutoka Afrika ya Kusini unaonesha dhahiri mahusiano mazuri baina ya nchi hizo mbili, alisema mahusiano hayo yanafanya SUA kuwa sehemu ya kihistoria ambayo inaendelea kuenea siku hadi siku na kukitangaza Chuo.

"Spencer Hodgson alikuja miaka ya 79 akiwa na familia yake huku binti yake akiwa na umri wa miaka tisa (9) tu, hivyo alisoma hapa kwa kuwa waliishi hapa. Hapo utaona ni namna gani ujio wao umeweza kutusaidia kujua mambo mengi zaidi na ya faida ya kutuwezesha kuendelea kuitunza sehemu hii ya kihistoria. Hivyo tu, bali wageni wanapoendelea kuja chuoni kwetu tunajitangaza pia kwa kuwa sisi ni sehemu ya historia hiyo kwa kuwa tupo kwenye eneo hili", alisema Dkt. Karugila.

Ugeni huo mbali na kutembelea majengo mbalimbali waliyokuwa wanayatumia kipindi hicho cha kupigania uhuru kama Ukumbi wa Nelson Mandela Freedom Square, pia walitembelea makaburi ya Wapigania Uhuru wa Chama cha ANC.



*Rasi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi (CoNAS) Dkt. Geoffrey Karugila akiwa na wageni kutoka Afrika ya Kusini.*





*Wanafunzi wa Mwaka wa Tatu wa Shahada ya Usimamizi wa Wanyamapori kutoka SUA wakiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na Kilele cha Uhuru katika Mlima Kilimanjaro kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo*








# SUA toeni elimu mliyoipata ya tahadhari na kukabiliana na majanga - Mkaguzi wa Jeshi la Zimamoto

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Morogoro limewataka wafanyakazi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambao wameshiriki mafunzo ya kukabiliana na majanga mbalimbali kuwa mabalozi wazuri na kuielimisha jamii namna ya kukabiliana na hali hiyo inapojitokeza.

Akizungumza katika mafunzo ya siku mbili yaliyofanyika katika Kampasi ya Edward Moringe Sokoine kuazia Mei 20, 2024 Mkaguzi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoa wa Morogoro Veronica John alisema Jeshi hilo linapofanyakazi ya uoakoaji hakuna gharama yoyote inayotozwa kwani huduma zote zinatolewa bure.

Alisema ni vyema washiriki kuzingatia kwa makini mambo yote walikayojifunza hasa tahadhari katika makazi na namna bora ya kukabiliana na majanga yakiwemo ya moto ambayo hugharimu maisha na mali za watu.

Aidha aliwataka wananchi kuachana na ujenzi holela ambao unasababisha kuchelewa kwa waokoaji kufika katika eneo lilitokea janga la moto na badala yake jamii ishirikiane na Jeshi la zimamoto na uokoaji katika uandaaji wa ramani za ujenzi ili kuwa na mpangilio mzuri wa majengo utakaowezesha uwepo wa miundombinu rafiki.

Kwa upande wake Jumanne Yusuph, Mrakibu Msaidizi wa Polisi Wasaidizi SUA alilipongeza Jeshi la Zimamoto na uokoaji kwa kutoa mafunzo ya kinga na tahadhari kwa wafanyakazi SUA na ametoa wito kwa wafanyakazi wote waliopata mafunzo hayo waende kutoa elimu kwenye jamii kuanzia ngazi ya familia na hasa kwa watoto ili kusaidia kuongeza tahadhari, kupunguza na kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza.

Nae Lucas Iyera mshiriki katika mafunzo hayo aliupongeza uongozi wa Chuo kwa kushirikana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuandaa mafunzo hayo ambayo yanasaida kuwakumbusha namna mwananchi anaweza kuchukua tahadhari katika kujikinga na majanga mbalimbali yakiwemo ya moto.






*Wanafunzi wa SUA wakishiriki bonanza la michezo katika kuhamasisha upimaji wa afya kwa magonjwa yasiyoambukiza.*














*Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wakiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Udzungwa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.*


**Jarida limetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano na Masoko

S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania

**Simu:** 255-023-2640006/7/8/9,

**Baruapepe:** communicationandmarketing@sua.ac.tz


**Ardhi ni Hazina**